# CHUO CHA KUMBUKUMBU YA MWALIMU NYERERE

**MAHAFALI YA ISHIRINI (20) KAMPASI YA KIVUKONI, MAHAFALI YA KUMI (10) KAMPASI YA KARUME - ZANZIBAR NA MAHAFALI YA TATU (3) KAMPASI YA PEMBA KWA MWAKA 2025**

Mkuu wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere anawatangazia wanafunzi waliohitimu masomo yao katika mwaka wa masomo 2024/2025 kwamba Mahafali katika kampasi zake zote tatu yatafanyika kama ifuatavyo: Kampasi ya **Kivukoni jijini Dar es Salaam** ambayo ni **Mahafali ya ISHIRINI** yatafanyika siku ya **Ijumaa tarehe 28 Novemba 2025,** Kampasi ya **Karume - Zanzibar** ambayo ni **Mahafali ya KUMI** yatafanyika siku ya **Jumatatu tarehe 1 Desemba, 2025 na kwa Kampasi ya Pemba ambayo ni Mahafali ya TATU** yatafanyika **siku ya Jumanne tarehe 2, Desemba 2025. Mahafali kwa Kampasi zote zitaanza saa TATU ASUBUHI (03:00).**

**Wahitimu wa Kampasi zote wanatakiwa kuzingatia yafuatayo:**

1 Kuchukua Majoho kwa Kampasi ya Kivukoni ni kuanzia **Jumatatu, tarehe 24.11.2025 hadi Alhamisi, tarehe 27.11. 2025,** kwenye ofisi namba 115 – Jengo la Uhuru; **Kampasi ya Karume - Zanzibar** majoho yatatolewa kuanzia siku ya **Alhamisi tarehe 27.11.2025 hadi siku ya Jumapili tarehe 30.11.2025;** na Kwa **Kampasi ya Pemba,** majoho yatatolewa **kuanzia tarehe 30.11.2025 hadi 1.12.2025.** Majoho yatatolewa kuanzia **4:00 asubuhi hadi saa 9:00 alasiri** kwa Kampasi zote na kuwa **Majoho hayatatolewa siku ya mahafali.**

2. **Malipo yote ya kulipia majoho yalipwe kwa kutumia mfumo wa kielektroniki (Control Number).Gharama ya Joho ni kiasi cha shilingi 40,000 (ELFU AROBAINI TU).**

3. Majoho sharti yarejeshwe Chuoni kabla ya **tarehe 6 Desemba, 2025 kwa Kampasi zote.** Vinginevyo **faini ya shilingi 10,000/=** itatozwa kwa siku kwa yeyote atakayechelewa kurudisha joho hilo.

4. Zoezi la namna ya kupokea vyeti **(Rehearsal**) litafanyika **Alhamis, tarehe 27 Novemba, 2025** kuanzia **saa 6.00 mchana kwa Kampasi ya Kivukoni,** na mahafali yatafanyika katika uwanja wa Mpira **Kampasi ya Kivukoni.** Kwa **Kampasi ya Karume-Zanzibar** zoezi hilo litafanyika **Jumapili**, **tarehe 30 Novemba, 2025** kuanzia **saa 4:00 asubuhi** katika uwanja wa mahafali Chuoni hapo, na kwa **Kampasi ya Pemba Rehearsal** itafanyika siku ya Jumatatu tarehe 1.12.2025 katika viwanja vya Kampasi ya Pemba Pujin, Chakechake Pemba.

**Mhitimu atakayeshindwa kuhudhuria zoezi hilo la rehearsal, HATARUHUSIWA kushiriki katika Mahafali.**

5. Kila mhitimu atapaswa kujigharamia usafiri, malazi na chakula.

6. Kusanyiko la Wahitimu wote **(**yaani **CONVOCATION)** waliosoma katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere litafanyika katika Kampasi ya Kivukoni jijini Dar es Salaam siku ya **Alhamis, tarehe 27 Novemba 2025** katika Ukumbi mpya wa Mihadhara **(NEW LT**) chuoni hapo kuanzia saa 4:00 asubuhi hadi saa sita mchana.

7. **WASHIRIKI WOTE WA MAHAFALI WANATAKIWA KUTHIBITISHA USHIRIKI WAO KATIKA OFISI YA MITIHANI KABLA YA tarehe 27 Novemba, 2025 kwa kupiga simu namba zifuatazo: 0679907412, 0782405552 na 0762020129**

**NYOTE MNAKARIBISHWA**

Mkuu wa Chuo,
Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere,
S.L.P. 9193,
**DAR ES SALAAM.**
Simu: +255 22 2820041/ 2820045/ 2820047
Faksi: +255 22 2820816
Barua pepe: rector@mnma.ac.tz